

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**

Cable: ELIMU DAR ES SALAAM.  
Simu: 2110146, 2110150/2, 211679.  
Telex: 242741 Elimu Tz.



S. L. P. 9121,  
DAR ES SALAAM.

Tarehe: 20/02/2010

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**MAMLAKA YA ELIMU TANZANIA (TEA) YAPATA MKURUGENZI MKUU MPYA**

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Mhe. Profesa Jumanne A. Maghembe amemteua Bibi Rosemary A. Lulabuka kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) kuanzia tarehe 1 Feburuari, 2010.

Waziri Maghembe amefanya uteuzi huo kwa mujibu wa Sheria ya Mfuko wa Elimu Tanzania Namba Nane (8) ya mwaka 2001 iliyoanzisha Mamlaka ya Elimu Tanzania, kwa kuzingatia kifungu cha 9 (i) kikisomwa kwa pamoja na Jedwali Na 2 kifungu cha kwanza.

Bibi Lulabuka ana Shahada ya Uzamili ya Utawala wa Biashara (Master's Degree in Business Administration) na ni "Certified Public Accountant" (CPA-T).

Kabla ya Uteuzi huo Bibi Lulabuka amekuwa akikaimu nafasi hiyo tangu Mei, 2009 na alikuwa Mkurugenzi wa Utawala na Fedha wa mamlaka hiyo. Aidha, Bibi Lulabuka amewahi pia kufanya kazi katika Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) akiwa Mhasibu Mwandamizi.

Bibi Lulabuka anachukua nafasi iliyoachwa wazi na Bibi Mercy Sila aliyeteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Mkuu wa Wilaya ya Arumeru Aprili, 2009.

Hamisi O. Dihenga  
**KATIBU**